# JARIBIO LA MTIHANI WA BARINGO

## DARASA LA NANE - MWAKA 2019

## KISWAHILI : LUGHA

**MUDA: SAA 1 DAKIKA 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala siyo katika karatasi hii ya maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**

   **JINA LAKO**

   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano:-**

    **Katika kartasi ya maswali:**

    **30. Jaza pengo:** _____ ni mti ambao magome yake hutumia kama viungo katika mapishi.

    A. Mdalasini
    B. Karafuu
    C. Pilipilimanga
    D. Iliki

    **Jibu sahihi ni (A) (Mdalasini)**

    **Katika karatasi ya majibu:**

    16 [A] [B] [C] [D] 22 [A] [B] [C] [D] 25 [A] [B] [C] [D] 30 ~~[A]~~ [B] [C] [D] 35 [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 30, kisanduku chenye herufi A ndicho kilichochorwa kistari.
11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Karatasi hii ina maswali 50 iliyopigwa chapa.**

**FUNGUA UKURASA**

***Chagua jibu lifaalo zaidi kujazia vihasho kuanzia nambari 1-15***

Endapo mtu ____1____ mahali pa kulala ____2____ maskani yako ____3____ nafasi utamwita ukamwonyeshe chumba cha kulala bila ____4____ kodi na hata ____5____ utampa bila malipo. Ukalimu huo ni ____6____ sana lakini mkarimiwa asiwe mtu wa ____7____ hayo awezapo kuepa ____8____ awe mtu ____9____ kutendewa.

| | A | B. | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ana | hana | una | kuna |
| 2. | nawe | naye | nao | nayo |
| 3. | ina | zina | yana | kuna |
| 4. | kumtoa | kumtolesha | kumtosha | kumtoza |
| 5. | mamkuli | maankuli | maakuli | makuli |
| 6. | mzuri | nzuri | uzuri | vizuri |
| 7. | kutendewa | kutenda | kutendea | kutendwa |
| 8. | ila | ili | hila | hili |
| 9. | awezayo | awezae | awezaye | awezao |

Vile ____10____ vilipohisi hatari vikatifua. ____11____ kuwafuata wale wenzao waliokuwa wamepotelea ____12____. Hata hivyo ____13____ yule hakuvipa ____14____ wa kutoweka. Mara ile alilenga ____15____ na kuuachilia ukaingia vilivyokuwa katika shabaha yake. Akawa ameliangamiza jangili lile.

| | A | B. | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 10. | vijana | viwete | viumbe | vifaru |
| 11. | Mbiu | Mbio | Mbweu | Vumbi |
| 12. | gizani | kwa gizani | katika gizani | giza |
| 13. | msasi | mzazi | msazi | mzasi |
| 14. | ñafasi | wasaa | saa | siku |
| 15. | ringu | jiwe | mkuki | bunduki |

***Jibu maswali kulingana na maagizo***

16. Andika kwa wingi
Ukuta mwingine uliojengwa umebomoka.
A. Kuta zingine zilizojengwa zimebomoka.
B. Nyuta nyingine zilizojenwa zimebomoka.
C. Kuta nyingine zilizojengwa zimebomoka.
D. Ukuta mwingine uliojengwa umebomoka

17. Badili sentensi hii iwe katika kauli taarifa
"Tutalima sana mwaka huu mkulima alisema
A. Mkulima aliosema tutalima sana mwaka huu
B. Mkulima alisema kuwa mwaka huu watalima sana
C. Mkulima alisema kuwa wangelima sana mwaka huu.
D. Mkulima alisema kuwa mwaka huu watalima sana

18. Anayetunza fedha au hazina ni mhazini
Anayetunza maktaba pamoja na vitabu vya maktaba ni?
A. Katiba B. Mkataba
C. Hatibu D. Mkutubi

19. Kama juzi ilikuwa Ijumaa tarehe sita mtondo itakuwa siku gani na tarehe ngapi?
A Jumapili tarehe nane
B. Jumatano tarehe kumi na moja
C. Jumanne tarehe kumi
D. Alhamisi tarehe kumi na moja

20. Chagua nomino dhahania
A. Urembo B. Mtoto
C. Mtakatifu D. Kucheza, cheza

21. Mtuuzi hodari wa mashairi huitwa_______?
A. Manju B. Mshenga
C. Malenga D. Muhiwa

22. Kikembe cha ngamia ni___________
A. kinengwe B. nirihi
C. kinda D. saraka

23. Kipi ni kielezi katika sentensi hii?
Mwalimu hodari amemchapa vibaya sana
A. Mwalimu B. Hodari
C. Vibaya sana D. Amemchapa

24. Yape maumbo haya majina
A. kopa, Hori wimbi ,tanki
B. Kopa, tumbomkate,wimbi,mcheduara
C. Kopa ,hori, mshazari ,tao
D. Kopa, hori, wimbi, hilali

25. Kamvika mtu kilemba cha ukoka ni:-
A. Kumpa sifa asizo stahili
B. Kumsema kwa mafumbo
C. Kumchafulia jina
D. Kumfanyia ishara ya dharau

**Chagua kundi sahihi la majina halisi ya kisarufi. Yaliyopigwa mstari katika mpangilio huu wa sentensi**

26. Mtoto yule aliye anguka vibaya ni wangu mimi
A. Kivumishi, kimilikishi, kielezi, jina
B. Kiashiri, kielezi, kiilikishi, nafsi
C. Kielezi, Kivumishi, Kirejeshi, Kiima
D. Kitenzi, Kiulizi, kiunganishi, kihusishi

**Jaza pengo kwa nomino inayotokana na nomino iliyipigwa mstari**

27. ________ yangu ana usuhuba mkubwa mno.
A. Shaibu B. Sahibu
C. Saibu D. Shahibu

28. Sentensi ipi isiyo sahihi?
A. Sisi ndisi tulishinda kwenye kandanda
B. Wao ndio walipata ushindi wa kandanda
C. Nyinyi ndinyi mliopata ushindi wa kandanda
D. Wewe ndiye uliyepata ushindi wa kandanda

29. Tamko la kumpa pole mtu aliyefikia na mshiba mkubwa kama vile kifo ni
A. makiwa B. pole
C. hayati D. hewala

30. Jimbi ni kuku dume. Aidha beberu ni kwa
A. mbuzi dume B. ng'ombe dume
C. nguruwe D. kuku jike.

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu swali 31 - 40**

Safari sio kifo wasanii wametuimbia. Lakini safari nyingine ni vigumu kuzipanga sembuse kuzitia maanani. Fikiria juu sa safari za angani.

Angani kuwa vitu na viumbe ainati kati ya vitu hivi ni sayari iitwayo dunia, tunamoishi. Wanasayansi wametudhihirishia dhahiri kuwa angani kuwa sayari tisa. Hizi ni Dunia. Zaibaki, Mirihi, Mshtarii, Zohali, Saratani, Kausi na Utadi.

Je, uliwahi kusikia hapo kale kulikuwa mtu na mwanawe waliotengeneza mabawa na kujaribu kufika angani? Wanasayansi na wataalamu wa anga wa zama walijaribu tangu miaka nenda miaka rudi kusafiri angani lakini ng'a, hawakufua dafu hata hivyo. Hawakata tama.

Hauchi hauchi unakucha. Mnamo mwaka elfu moja mia kenda sitini na moja, yuri gagarini kutoka Urusi alikuwa na mtu wa kwanza kusafiri katika anga walirusha vyombo vya angani, wakatumia kamera na vifaa hadi duniani. Hata wanyama kama mbwa walipelekwa katika anga za juu!

Baadaye, majaribio yalifuatana mithili ya usiku na mchana. Mwishowe, chombo maarufu cha angani kilichoitwa Apollo II kilirushwa na kutua salama kwenye mwezi. Ndani ya chombo hicho kulikuwa na

watu watatu. Neli Amstrong na mwenzake Eldin Aldrin walikuwamo. Waliteremka na kukanyaga chini mwezini walijaribu kulala lakini walishindwa.

Neli Amstrong ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kushuka kutoka chombo cha Apollo II na kuweka alama ya wayo wake juu ya mwezi. Dimbui la mayi lilijitokeza juu ya uso wa mwezi! Hawakuamini.

Baada ya wanaanga hawa kutua mwezini waliikita bendera ya nchi yao. Bendera hii haikupeperuka kwa sababu hakukuwa na upepo. Hata inasemekana kwambahuyu Aldrin alijaribu kuruka lakini alieleaj uu juu kiajabu! Kumalizika kwa hayo yote, wanaanga hao walirudi na kuungana na mwenzao Mike Collins aliyebaki katika chombo hicho.

Kufikia wakati huu, wanasayansi na wataalamu waliobakia mabuku ya taaluma hii ya angani wamejaribu kila uchao kutua mwezini. Wengine hata walijaribu kupeleka mimea huko.

Wanasayansi hawa wamejaribu kutupa vyombo vya kisayansi kama roketi kwenda sayari nyingine. Hii imewezesha wanaanga na wanasayansi na hata sisi kina yake kuelcwa mengi kutoka sayari hizi.

Wanasayansi hawa na wataalamu wa angani wataweza kupaa na kutua kwenye sayari nyingine kama zuhura, mihiri na mushtarii kwani penye nia pana njia. Si ajabu wanadamu wakawa wakiabiri kutoka sayari moja hadi nyingine!

31. Ni kichwa gani kinachofaa habari hii?
A. Wezimtanda
B. Waliobobea katika teknologia
C. Teknologia
D. Wezitalakalishi

32. Safari nyingine hazipangiki sembuse?
A. Wajadi walitumba
B. Zina kifo
C. Ni vigumu kuzipanga
D. Kuzitia maanani

33. Sayari anamoweza kuishi binadamu ni
A. Zebaki B. Dunia
C Zuhura D. Mushtarii

34. Je, adiwasi yule na mwanawe waliojaribu kuruka kwenda angani walifua dafu?
A. Ndio B. Haikueleza
C. La D. Haijulikani

35. Idadi ya watu walioteremka walipofika kwenye mwezi ni
A. watatu B. mmoja
C. wote D. wawili

36. ________ ni jina la mtu wa kwanza kusafiri angani.
A. Yuri Gagaarini B. Neil Armstrong
C. Edwin D. Aldrin

37. Dunia yetu ni mojawapo ya
A. Sayari
B. Nyota
C. Zebaki
D. Ulimwengu

38. Waanga walifanya nini baada ya kutua mwezini
A. Waliikita bendera ya nchi yao
B. Bendera haikupepcruka kwa sababu hakukukuwa na upepo
C. Waliwaza sana
D. Aldrin alijaribu kuruka lakini alielea

39. Ni chombo gani wanasayansi wamepeana kusafiria zile sayari zingine?
A. Roketi
B. Ndege
C. Kamera
D. Dunia

40. Methali nyingine iliyo na maana sawa na penye nia pana njia ni
A. Dawa ya moto ni moto
B. Penye urembo pana urimbo
C. Pole pole ndiyo mwendo
D. Haraka haraka haina baraka

***<u>Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50</u>***

Hakuna shaka kwamba tumekuwa na maendeleo makubwa hapa nchini . Ashahidi wa aina mojawapoya maendeleo haya ni shule ambazo zimetapakaa kote nchini. Matokeo ni kuwa Watoto wengi huishi karibu na shuleni wanakosomea. Heko kwa serikali yetu kwa jinsi inavyo yajali maslahi ya raia wake. Ni bahati mbaya tu kinyume cha mambo. Hakuna vipovu na viziwi ambao kazi yao ni kulaumu. Hawa ni watu wasioridhika kutokana na uchoyo yao, wala hatuna ya kuwajali kwa sisi ambao tumeridhika na maendeleo haya tumepata kuyaona manufaa yake.

Wanafunzi wanaoishi karibu na shule hawahitajiki kulipa nauli yoyote lakini kuna wengine wachache ambao kwa sababu fulani hujikuta wanaishi mbali sana na wanakosomea. Isitoshe, inawazekana kuwa kati ya shuleni na makwao kusiwe na huduma ya usafiri. Hao huwa hawana budi kurauka na kupiga mguu ili wafike shuleni kwa wakati unaofaa.

Watoto ambao wazazi wao wanajimudu hawalazimiki kuondoka nyumbani mapema lakini wazazi wa watoto hawa wanatakikana wajue shinda za usafiri zinazowapata wenzao na kuwasaidia kila wanapoweza kufanya hivyo. Mbali na hayo, hawa wanafunzi wanakula kiasi cha kusinzia darasani baadaye, kuna wenzo ambao hungurumwa tuna matumbo.

41. Pamekuwa na maendeleo makubwa hapa nchini kwa sababu.
   A. Shule zimetapakaa kote nchini
   B. Serikali inatekelaza wajibu wake
   C. Watu wengi huishi karibu na shule
   D. Wananchi ni wazalendo wanaojali nchi yao.

42. Kulingana na habari ni kina nani "vipofu na viziwi"
   A. Watu ambao hawaoni wala kusikia
   B. Watu wasioridhika kwa sababu ya uziwi wao
   C. Watu wasiotosheka kwa sababu ya ubinafsi wao
   D. Ni watu wasioona wala kusikia kwa kutotosheka kwao

43. Matokeo ya shule kutapakaa kote nchini ni kuwa
   A. Wanafunzi wengi hawana haja ya kujichosha kwenda shule.
   B. Wanafunzi hawakosi kwenda shule hata siku moja
   C. Wanafunzi hawana haja na kushindana
   D. Wanafunzi wanasoma shule nzuri ambazo ni nyingi.

44. Wanafunzi wengine hungurumwa na matumbo kwa sababu
   A. Kushiba sana
   B. Kusikia njaa
   C. Kuchafukwa na tumbo
   D. Kusinzia darasani

45. Kusema zimetapakaa ni kusema.
   A. Zimejengwa
   B. Zinasomewa
   C. Zinapatikana
   D. Zinaanzishwa

46. Hatuna haja na kuwajali ni kusema.
   A. Tusiwapuuze
   B. Tusiwalaumu
   C. Tuwalaumu
   D. Tuwapuuze

47. Kulingana na habari hii, tunashauriwa kuwa tumebahatika.
   A. tuwasaidie wenzetu tuwezapo kufanya hivyo
   B. Tufike shuleni mapema
   C. Tufurahie wenzetu
   D. Tuwashukuru wazazi kila tuwezapo

48. Kusema hawana budi kurauka ni kusema
   A. Ni lazima waondoke mapema asubuhi
   B. Si lazima waondoke mapema asubuhi
   C. Hawalazimishwi kuondoka mapema asubuhi
   D. Ni lazima wafike shule kwa wakati unaofaa

49. Kulingana na habari hii kujimudu ni
   A. Kuharibu fedha
   B. Kupata mkopo
   C. Kukimbilia maisha
   D. Kuwa na uwezo

50. Mada ya habari hii ni kuhusu
   A. Mwanafunzi kushinda na njaa
   B. Mafanikio yanayofurahiwa nchini
   C. Watoto kusoma kote nchini
   D. Wenye mali kuwasaidia maskini.